# Hotuba Ya Mkuu Wa Chuo Kikuu Kishiriki Cha Ushirika na Biashara Prof. S.A. Chambo Kufungua Kongamano la Kuadhimisha Siku ya Ushirika Duniani Chuo Kikuu Kishiriki Cha Ushirika na Biashara Moshi, Tarehe 28-06, 2006

Mwenyekiti wa Kongamano,

Washiriki, Wataalam,

Wanaushirika,

Mabibi na Mabwana.

Natanguliza shukrani zangu kwa kunikaribisha kufungua Kongamano hili muhimu la kuadhimisha Siku ya Ushirika Duniani. Nafahamu kuwa kilele Cha siku hii muhimu, ni Jumamosi tarehe 01/07/2006. Sherehe za Siku hii kitaifa, zitafanyika huko Tabora ambako chuo chetu kinashiriki kikamilifu,

Lakini sisi kama waelimishaji, watafiti na washauri wa Ushirika, tuna jukumu rasmi la kisheria, kisera na kitaalam la kufanya Kongamano hili la siku moja kila mwaka wakati wa sherehe hizi.

Ni katika msingi huo, leo nitajaribu kuzungumzia masuala ya ujenzi wa Ushirika mpya na endelevu hapa Tanzania, na jinsi gani ushirika unavyochangia katika kuleta amani endelevu nchini.

Mada kuu ya Siku ya Ushirika Duniani ni "Jenga Amani Kupitia Ushirika". Maelezo yangu katika ufunguzi wa Kongamano hili hivi leo, nitajaribu kujibu maswali matatu:
La kwanza ni Je kuna uhusiano kati ya Ushirika na Amani?

Swala la pili, ni kuwa kama upo uhusiano kati ya Ushirika na amanıı je kuna mafanikio na vikwazo kuhusu uhusiano huo katika nchi yetu ?

Swala la tatu na la mwisho ni kuwa Je sisi wadau wa Ushirika tufanyeje ili kuimarisha uhusiano kati ya Ushirika na amani.

Mwenyekiti,

Ushirika ni mfumo wa ki-organizesheni ambao unaundwa na watu wenye nia ya kuutumia Ushirika huo kujiletea mafao au maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Watu wanaounda Ushirika huoı wanajiunga kwa hiari yao na ya kwamba wanakubaliana na masharti ya kiutendaji na kanuni zake ambazo zinakubalika kimataifa.

Amani, ni hali ya utulivu na isiyo na migongano ya mtu na mtu, tabaka na tabaka, kati ya jinsi, kabila na kabila na kati ya taifa moja na lingine.

Hali ya utulivu inatokana na msingi kuwa mifumo ya uzalishaji mali, ugawaji wa mali na maslahi mengine, na imejengwa katika misingi ya usawa. Usawa na haki vinaanzia kwenye kumiliki njia za uchumi za uzalishaji, usambazaji na utumiaji.

Mfumo wa kibepari ni mfumo unaojenga mahusiano hasi ya kijamii na ukiachwa uendelee bila kuguswa au kuhojiwa na kubadilishwa, athari zake ni kuigawa jamii katika makundi ya wenye mali wachache na masikini wengi.

Miaka 152 iliyopita, mfumo wa Ushirika ulianzishwa na watu wa tabaka la wasio na mali na wafanyakazi wa hali ya chini. Mfumo wa Ushirika ulianzishwa ili kutoa baadhi ya majibu kwa masuala ya mgawanyiko wa jamii ki-uchumi na kisiasa. Mfumo wa Ushirika kwahiyo, una mantiki ya kihistoria ya kuleta usawa na haki katika umiliki wa mali na rasilimali na kujaribu kupunguza makali ya migawanyika ambayo ingeweza kutokea kama mfumo wa kibepari ungeachwa uendelee kama ulivyo.

Mgawanyo wa kumilki mali si şuala la nchi moja moja tu, bali kukua kwa mfumo wa kibapari kulikotokea karne za 19 na 201 na baadaye kuingia utandawazi wa kibepari ambao katika karne

ya 21 utaigawa dunia kati ya nchi tajiri sana kwa upande mmoja na nchi masikini sana kwa upande mwingine. Uchumi wa utandawazi wa kibepari ukiachiwa uendelee wenyewe tu, amani itatoweka vita zitaanza ndani ya nchi na kimataifa.

Kwa hiyo, kuna mahusiano makubwa sana kati ya Ushirika na amani kwa vile Ushirika unazungumzia haki ya watu wengi kumiliki mali, watu wengi kushirikiana katika kuwekeza, haki sawa ya kuchangia rasilimali na haki sawa ya kugawana matokeo ya uzalishaji.

Kanuni kuu za Ushirika ni usawa, kujitegemea na maongozi ya kidemokrasia. Kanuni hizi kuu, zinazungumzia namna ya kujenga amani kati ya watu, ndani ya nchi na kimataifa.Ndiyo maana hivi leo tuna mtandao wa vyama vya ushirika duniani yaani ICA . Mtandao huo unatoa angalizo kuwa bila ushirika amani na uhuu viatakuwa mashakani duniani.

## 2.0 Je kama kuna uhusiano kati ya Ushirika na kuwepo kwa amani, kunaweza kuwa na fursa zipi na vikwazo vipi vya kuimarisha amani hapa Tanzania.

### 2.1 Fursa

Historia ya maendeleo ya Tanzania, ina mguso mkubwa sana wa maendeleo ya Ushirika.Tanzania, imekuwa ikijulikana kama nchi ya amani na utulivu mkubwa. Tunaweza kusema kuwa amani na utulivu wa Tanzania umechangiwa na kuwapo kwa Ushirika. Chimbuko la Ushirika nchini Tanzania lilikuwa kuigania haki ya kupata bei nzuri ya mazao ya biashara. Ushirika ulipoanza na kukubalika kwenye maeneo ya Pamba, Kahawa, Tumbaku na Korosho, wananchi walianza kuongeza mapato yao, haki ilitendeka na uchumi kwa ujumla ulianza kukua kwa haraka.

Mafanikio ya Ushirika kwenye mazao ya biashara yaliihamasisha serikali kuanzisha ushirika kwenye meneo ya chakula nchi nzima.

Pili, maeneo ambako Ushirika ulishamiri, uchumi wa soko ulijengeka na hadi leo, maeneo hayo yana maendeleo makubwa kiuchumi kuliko maeneo yenye histori fupi ya Ushirika. Maeneo ya

uzalishaji wa chakula kwa mfano, Uchumi unaotegemea fedha ni mfunyu mno, na wananchi wana fursa finyu sana za kupata fedha.

Tatu, maeneo yenye historia ndefu ya Ushirika yana wasomi wengi na wenye uwezo mkubwa wa kuzalisha mali kuliko yenye historia fupi ya Ushirika. Maeneo yote yenye historia ndefu ya Ushirika kulikuwa na ujenzi wa shule za sekondari za nguvu za wananchi za siku nyingi kuliko maeneo yenye Ushirika hasi. Watu waliosoma kiwango cha Sekondari wana fursa pana za kuingia katika uchumi wa soko huru ukilinganisha wahitimu wa darasa la saba. Ndiyo maana Hayani Mwalimu Nyerere alisema, fedha si msingi wa maendeleo, bali wape watu elimu bora na watakuwa na uwezo wa kuzalisha mali na kujenga uchumi kwa amani na utulivu.

Nne, maeneo yenye Ushirika wa siku nyingi ni rahisi kukubali mifumo mipya ya Ushirika kama vyama vya aina nyingine kama SACCOs na vile vya aina isiyo ya kilimo. Hii ina maana kuwa Ushirika ukiongeza fursa za kuongeza mapato, na amani itakuwako. Hoja ya msingi ni kuwa, **Ushirika ni asasi inayopanua fursa ya binadamu kuweza kufikia mafao ya kukidhi maisha yake ya kila siku. Binadamu ambaye hafikii mafao ya kukidhi hali yake duni ya maisha, huyo ni mteia mzuri sana wa kuunqa mkono machafuko ya aina ye vote nchini.**

**2.2 Vikwazo**

Pamoja na kwamba Tanzania ni nchi ya amani na utulivu, ukweli upo pale pale kuwa maumbile ya uchumi wake yanatakiwa yaangaliwe upya ili yaweze kukidhi mstakabali wa kuitetea na kujenga amani hiyo indelee kuwa endelevu. Sisi wote tunaamini kuwa vyama vya Ushirika peke yake haviwezi kuwa chimbuko la amani kamilifu ya taifa letu. Lakini ni ukweli wa wazi kuwa nchi yeyote ikiwa na vyama vya Ushirika endelevu na vinavyowashirikisha wananchi walio wengi na maskini, kuna uhakika kuwa wananchi hao watakuwa na uwezo wa kufikia na kukidhi mafao yao ya kuendesha maisha yao kila siku. Na hii itapunguza mianya inayoashiria kumomonyoka kwa amani.

Mara nyingi sasa, Rais Kikwete amekuwa akizungumzia kuwa mojawapo ya mambo muhimu ambayo serikali ya awamu ya nne itajikita, ni katika kuhakikisha kuwapo kwa fursa za kuongeza

mapato ya watanzania mmoja mmoja. Mkakati huu unaendana na malengo ya kuwapo kwa Ushirika. Ushirika ni mfumo wa kiasasi unaotoa fursa ya kujenga uchumi wa mwanachama mmoja mmoja kwa kutumia uchumi-vikundi. Hii ina maana kuwa kipimo cha mafanikio ya Ushirika hivi sasa, ni lazima kionekane katika ongezeko Ia mapato ya mwanachama mmoja mmoja.

Tunaposema tunakipongeza chama cha Msingi Mamsera kwa mafanikio waliyopata kwenye biashara ya Ushirika mwaka uliopita, tuna maana kuwa chama hicho kiliweza kufikisha bei ya Kahawa ya wastani wa shs. 1,850 kwa kilo na zaidi. Vile vile waliweza kugawa mafao ya mabadiliko ya thamani ya fedha za kigeni kwa shs. 4,000 kila mwanachama. Kwahiyo kwa taarifa hizi, wanachama wa chama cha Mamsera wameweza kuongeza mapato yao kupitia biashara ya Ushirika. Na wanachama waliweza kupata fursa ya kupima uwezo wa chama chao kupitia kigezo cha ongezeko Ia mapato.

Suala Ia kusema wanachama wamefaidika na huduma za Ushirika kwa ujumla wake limepitwa na wakati, Mfano wa Mamsera ni mmoja tu, viko vyama vingi vya msingi hapa Tanzania huko Mbinga, Kigoma, Mbozi na sehemu nyingine ambao wamepata mafanikio hayo. Tunachopenda kuona kwa mfano, ni kuwa chama cha msingi Mamsera, wamelipa mkopo wao wa zaidi ya shs millioni zaidi ya 138, 000, 000 wa fedha za kununulia mazao kwa haraka sana kiasi kwamba badala ya kulipa riba ya shs millioni 16, walilipa riba ya jumla ya shs 2, millioni tu. Huu ndio mwanzo wa ushirika mpya.

Ushirika mpya unajengwa kwa misingi ya uwazi na ukweli na ya kwamba wanachama wanachotaka kuona ni kubaini kuwa mapato yao yanaongezeka kutokakana na Ushirika wao mwaka hadi mwaka.

Matukio mengi ya ujambazi ni kielelezo cha ufinyu wa fursa za kiuchumi katika nchi, na ni tishio kwa amani. Lakini nchi yetu ikijenga vyama vya Ushirika imara na vinavyoongeza mafao kwa idadi kubwa ya wananchi; hata mianya ya ujambazi itapungua. Hata hivyo, pamoja na hayo yote

yanayoonyesha kuwa Ushirika ni chimbuko mojawapo Ia amani, Je Ushirika hapa Tanzania unapata vikwazo gani usifikie lengo Ia kuchangia amani na utulivu kikamilifu?

Sababu ziko nyingi, lakini leo nitazungumzia vikwazo vinavyotokana na maudhui ya kihistoria, kukubalika ndani ya jamii, uongozi na mifumo kongwe ya Ushirika.

**i) Maudhui ya Kihistoria (Historical Context)**

Kipimo muhimu cha Juhudi za ujenzi wa Ushirika ni ongezeko na upanuzi wa vyama vya Ushirika kijiografia, kijamii na ki-sekta. Juhudi za kuongeza vyama vya Ushirika ni finyu mno kwa maana kuwa uhamasishaji wa kuanzishwa kwa vyama vipya umeachiwa serikali na asasi zisizo za kiserikali.

Hapa kuna matatizo ya aina tatu: Kwanza zama tulizonazo, vyama vya Ushirika haviwezi kuendelea kuanzishwa moja kwa moja na serikali. Dhana ya Ushirika kuanzishwa moja kwa moja na serikali inaashiria matatizo ya kifikra kuwa serikali ikivianzisha moja kwa moja, vyama vya Ushirika vitakuwa ni vyake na itabeba majukumu ya kuviendeleza hata bila kuwa na wanachama. Kwahiyo kinadharia, serikali haina tena jukumu la kuanzisha vyama vya Ushirika moja kwa moja. Lakini vile vile, hata kama ingekuwa na jukumu hilo, si rahisi serikali kuwa na mtandao wa kuanzisha vyama hivyo ngazi ya vijijini.

Serikali inachoweza kufanya ni kuunga mkono uhamasishaji, usimamizi wa Sheria, sera, kanuni na miongozo ya utawala bora.

Pili, asasi za kitaifa za Ushirika ambazo zingeweza kufanya kazi ya kuzalisha vyama vipya vya Ushirikaı hazina uwezo huo na hazina methodolojia muafaka ya kuhamasisha na kuzalisha vyama vipya vya Ushirika ndani ya jimii, ki-sekta na kijiografia.

Tatu, kama kazi ya kuanzisha vyama vya Ushirika itaachiwa asasi zisizo na kiserikali, nchi itakosa mkakati wa kitaifa wa ujenzi wa Ushirika kwa sababu asasi hizo zinaweza kuwa na malengo ya

muda mfupina pengine ya majaribio tu. Hata hivyo, napenda nibaini kuwa ziko asasi chache zisizo za serikali , ambazo zina malengo ya muda mrefu ya maendeleo ya ushirika hapa Tanzania.

Tunahitaji mkakati wa pamoja kati ya serikali, asasi za kitaifa za Ushirika na asasi zisizo za kiserikali ili kufikia malengo ya muda mrefu ya kuanzisha vyama vipya vya Ushirika endelevu nchi nzima.

Vikwazo vingine vinavyotokana na maudhui ya kihistoria ni pamoja na sheria ya Ushirika, ukaguzi na elimu ya Ushirika.

Sheria ya Ushirika ina vikwazo vingi ambavyo haviruhsu uanzishwaji na uandikishwaji wa vyama vya Ushirika kwa kasi kubwa. Wanaoandikisha wameshika fimbo ya kukwamisha, kuadabisha na kusanifu taratibu. Wananchi wanaotaka kuunda vyama vya Ushirika wanawekwa katika mzunguko wa njoo kesho, njoo kesho mpaka wanakata tama. Ukaguzi wa vyama vya Ushirika bado ni wa kizamani na hautoi fursa kwa wanachama kuona Umuhimu wa ukaguzi kama msingi wa utawala bora katika biashara ya Ushirika. Ukaguzi unaonekana ni utaratibu wa serikali wa kutafuta "wezi" wa mali za Ushirika na hauna mvuto wa kupendwa na wanachama na kuzitumia ripoti za ukaguzi kuboresha biashara yao.

Kwenye upande wa elimu kuna matatizo matatu: Kwanza elimu haitoi maudhui ya kuhamasisha wananchi kuunda na kuanzisha vyama vipya vya Ushirika. Pili kuna mchanganyiko wa matumizi ya dhana za Ushirika wa zamani na Ushirika mpya. Baadahi ya watoa elimu bado wanaamini dhana ya Ushirika wa zamani ambayo inasema bila mkono wa serikali hakuna Ushirika na vyama vya msingi kusubiri vyama vikuu viwauzie mazao. Na wengine wamebadilika na kuona na kufundisha Ushirika kama mfumo wa biashara ya uchumi vikundi na ya kwamba Ushirika biashara na wanachama kuukataa uchumi wa kujikimu na kuwa wajasiriamali ndilo lengo la Ushirika.

Tatu, hakuna mkakati wa pamoja wa Ushirika biashara kwa taasisi zote zinazotoa elimu ya Ushirika. Hii inawachanganya wananchi kuwa dhana ya Ushirika mpya na Ushirika biashara inaanzia wapi na inaishia wapi. Wanachama wanajiliza, je mkaguzi wa COASCO anapokuja kukagua vyama vya Ushirika anatumia hadidu za rejea za Ushirika wa zamani au mpya? Je ofisa Ushirika anapokuja kufanya "Inspection" anatumia dhana ipi ya ushirika ?Je yuko kwenye ushirika wa zamani au mpya ? Taarifa tunazopata ni kuwa bila kuongeza elimu, maofisa Ushirika watakuwa kikwazo cha kukua kwa ushirika mpya.

**ii) Uongozi na Ushirika Kukubalika Ndani ya Jamii**

Ili Ushirika uweze kuenea nchi nzima ndani ya jamii na kila eneo la nchi ya sekta, inategemea mifano mizuri ya utawala, uchumi na uongozi wa Ushirika uliopo. Wananchi wa kawaida, watapata motisha ya kujiunga na vyama vya Ushirika kama wataona mifano bora ya kutegemewa. Historia ya Ushirika nchini mwetu ilianza na Ushirika bora na chanya, lakini ikafuatwa na Ushirika hasi na hafifu. Matatizo ya kisera, sheria na uongozi, yamekuwa makubwa kiasi kuwa baadhi ya maeneo ya nchi yetu ukitaja neno Ushirika — moja kwa moja linapata tafsiri ya wizi, ubadhirifu, unyonge, ubabaishaji utapeli na meneno yote mabaya ya mahusiano ya kiuchumi.

Picha hii, ni kikwazo kikubwa sana na hasa tabia inayoonyeshwa na baadhi ya viongozi wa vyama vya Ushirika kuionyesha jamii kuwa uongozi katika Ushirika ni utaratibu wa kujilimbikizia mali na kwahiyo ni viongozi wa maisha katika Ushirika. Hali hii ni lazima ipigwe vita ili tujenge ari mpya na imani mpya kuhusu Ushirika katika jamii.

**iii) Mifumo Kongwe ya Ushirika**

Adui mkubwa wa ujenzi wa Ushirika na uwezo wa kuchangia katika amani' ni mifumo kongwe ya Ushirika usiobadilika na usiokwenda na zama za uchumi wa utandawazi wa kibepari. Bila kuifanyia uchambuzi wa kina utendaji kazi wa mifumo kongwe ya Ushirika, mifumo hiyo itaendele kuwa ya gharama kubwa na wanachama kujikuta wanaendelea kupoteza mapato na kuendelea kuwa maskini ndani ya Ushirika wao.

Uchumi wa soko huru, ni fursa ya kuhuisha mifumo kongwe ili kuruhusu kuibuka kwa Ushirika mpya. Ushirika mpya ni ule ambao wanachama wanabeba majukumu makubwa ya biashara ya Ushirika. Wanachama wanasimamia mlolongo wa thamani ya bidhaa zao hadi mnunuzi wa mwisho (value chain management). Ushirika mpya unadai upunguzaji wa gharama na ya kuwa vyama vikuu kufanya kazi nje ya barabara ya thamani ya biashara ya Ushirika. Vyama vikuu vishughulikie kujenga uwezo wa vyama vya msingi ili vyama hivyo vifanye biashara yenye faida kubwa pamoja na kuwaunganisha na kuwalinda katika mfumo wa biashara ya ubia kitaifa na kimataifa (Second Generation Cooperatives) Ushirika uliopangwa kisayansi na kisasa, utakidhi haja ya msingi ya kuongeza mapato kwa wanachama, kuwa chimbuko la ajira kwa vile mlolongo wa thamani ya mazao utapitia mifumo ya usindikaji na kuongeza thamani ya mazao. Haya yote yatasaidia kuongeza fursa za mfiko wa mafao kwa wananchi wengi kupitia mifumo ya Ushirika mpya.

Labda nichukue nafasi hii kueleza msimamo wetu kuhusu vyama vikuu vya Ushirika wa mazao. Mara nyingi dhana potofu imetumiwa kueleza nafasi ya Chuo Kikuu Kishirika cha Ushirika na Biashara kuwa Chuo hakipendi vyama vikuu. Nataka kusisitiza kuwa Sisi ni watetezi wa Ushirika wa aina zote na wa ngazi zote. Tunachohoji ni vyama vikuu vinavyoendelea na mifumo kongwe isiyobadilika na inayoshindwa kusimamia ufanisi wa biashara ya vyama vya msingi nje ya mlolongo wa thamani ya mazao, kama nilivyoeleza hapo juu.

**3.0 Nafasi ya Ushirika katika kuleta Amani endelevu Tanzania**

Ushirika una nafasi kubwa sana ya kuchangia maendeleo ya uchumi wa Tanzania. Ushirika unakidhi moja kwa moja mahitaji na malengo ya kitaifa na mikakati ya kujenga uchumi na kuondoa umaskini kama MKUKUTA na MKURABITA.

Ushirika ni mfumo wa kiasasi unaojikita katika kujenga uchumi wa mwanachama mmoja mmoja kwa kutumia mkakati wa uchumi vikundi: Kama tulivyoeleza hapo awali, ukitaka kupima mafanikio ya MKUKUTA, ingia ndani ya vyama vya Ushirika utaona jinsi ambavyo kwa kupitia taasisi hizo, wananchi wameweza kuongeza uchumi na kupunguza umasikini.

Kuna haja ya kufanya uwianishaji kati ya mkakati wa MKUKUTA na Ushirika.

Suala hili limebainishwa na mpango wa maboresho ya Ushirika na kuufanya Ushirika uwe wa kisasa zaidi. CRMP au Cooerative Reform and Modernizaton Programme. Programmu hii, inauweka Ushirika katika maudhui ya MKUKUTA• Kupitia MKUKUTA, mafanikio ya ushirika katika kujenga uchumi yanaweza kipimwa. Hata hivyo, CRMP, bado inaonekana kua dhana na zana ya serikali badala ya kuwa dhana ya muungano wa vyama vya ushrika nchini.

Vile, mkakati wa kurasimisha biashara Tanzania (MKURABITA) ni mkakati ambao kwenye maudhui ya Ushirika unatekelezeka moja kwa moja. Ushirika unaanza na wanachama mmoja mmoja wanaofahamu umaskini wao. Hata hivyo, huko nyuma, wanachama hawakuwa na utaratibu wa kurasimisha mali na biashara zao. MKURABITA ni mkakati muhimu sana kwa wanachama kwa sababu utawasaidia kupata zana za kutathmini mali zao na kuzirasimisha. Kama lengo kuu la Ushirika ni kuondoa umaskini, baada ya kurasimisha mali zao, MKURABITA itawasaidia kufanya tathmini kama mali zao zimeongezeka kutokana na Ushirika au la. Lakini vile vile MKURABITA utajenga mfumo wa wanachama kujiona katika maudhui ya kuwa wafanyabiashara.

Tunahitaji mikakati ya pamoja kuandaa taratibu na methodolojia za kuongeza Vyama vya Ushirika, elimu ya Ushirika biashara na Ushirika mpya., ukaguzi shirikishi na elimu ya kilimo biashara , akiba na mikopo biashara na ujenzi wa mifumo ya Ushirika mpya, na uongozi wa kijasiriamali ili Ushirika uwe na fursa pan aua kuchangia katika kuleta amani endelevu nchini mwetu.

Baada ya kusema haya, napenda kutamka kuwa kongamano la siku ya Ushirika Duniani limefunguliwa rasmi.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.